

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630

Nukushi: +255 (026) 2963629

Barua Pepe: [ps@utumishi.go.tz](mailto:ps@utumishi.go.tz)

Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma  
na Utawala Bora,  
Chuo la Taaluma Na. 1,  
Chuo cha Masomoya Biasharana Sheria,  
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),  
18 Barabaraya Mkalama,  
S.L.P. 670,  
**40404 DODOMA**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### WAHITIMU WA MAFUNZO YA UONGOZI WATAKIWA KUTUMIA VIZURI UJUZI WALIOUPATA ILI KUONGEZA UFANISI KATIKA UTENDAJI KAZI

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) amewataka wahitimu wa mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Masuala ya Uongozi kutumia vizuri ujuzi walioupata ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na hatimaye kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

Mhe. Dkt. Mwanjelwa (Mb) amesema hayo, alipokuwa akizungumza katika hafla ya kuwapongeza wahitimu wa Stashahada ya Juu ya Masuala ya Uongozi iliyofanyika katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam.

Mhe. Dkt. Mwanjelwa amesema anatarajia wahitimu hao kuwa mfano bora wa kuigwa katika jamii kwa kusimamia vema masuala ya utawala bora, haki za binadamu, utawala wa sheria huku wakionyesha uzalendo na ufanisi wa hali ya juu katika shughuli zao za kila siku.

“Nina imani kuwa mafunzo haya yamewabadilisha kifikra na kimtazamo katika masuala yote yanayohusu uongozi na mmekuwa na uelewa mpana utakaobadili utendaji kazi wenu kutokana na programu hii iliyofundishwa na wataalamu wabobezi wa hapa nchini na nje ya nchi,” Dkt. Mwanjelwa amesisitiza.

Mhe. Dkt. Mwanjelwa ameongeza kuwa, serikali inategemea kuona kwa vitendo kile walichojifunza darasani kwa kipindi cha mwaka mmoja ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa kuzingatia uzalendo na uadilifu mkubwa na kuwa na uongozi wa kimkakati kwa kusimamia vizuri rasilimaliwatu na rasilimali fedha.

Akizungumza kwa niaba ya wahitimu, Bi. Neema Mwakalyeye ameahidi kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Mhe. Dkt. Mwanjelwa na kusema kuwa watakuwa viongozi bora wanaopenda mabadiliko chanya ili kutimiza dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Aidha, ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuruhusu watumishi kuhudhuria mafunzo hayo na Serikali ya Finland kwa kudhamini na hatimaye kufanikisha uwepo wa mafunzo hayo nchini Tanzania.

Jumla ya wahitimu 33 wakiwemo baadhi ya viongozi wastaafu wa serikali na viongozi waandamizi serikalini walitunukiwa vyeti vya Stashada ya Juu ya Masuala ya Uongozi yanayotolewa na Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Chuo cha AALTO cha nchini Finland.

IMETOLEWA NA;  
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**  
**OFISI YA RAIS (UTUMISHI)**  
TAREHE 10 APRILI, 2019